SAYYID MUHAMMAD BIN SAYYID AHMAD BADAWY

SHARIFF DINI

SAYYID MUHAMMAD BIN SAYYID AHMAD BADAWY

SHARIFF DINI

Jina lake khalisi ni Sayyid Muhammad ibn Sayyid Ahmad Badawy ibn Habib Swaleh ibn Alwy Jamaalu Layl. Alipewa Laqab ya Shariff Dini utotoni mwake

WAZAZI WAKE

BABA

Babake ni Sayyid Ahmad Badawy

(Mwenye Badawy), mtoto wa Habib Swaleh ibn Alwy Jamaalu Layl.

MAMA

Mamake ni Aisha(Mama Khale) binti

Shaikh Abdallah ibn Muhammad Bakathir Al-Kindy.

ALIPOZALIWA

Sharifu Dini alizaliwa katika mji wa Lamu mwaka wa 1910 AD (1330 AH) na **ni mtoto wa pili wa kiume wa Mwenye Badawy** baada ya ndugu yake mkubwa Sayyid Ali ibn Sayyid Ahmad Badawy.

Alikuwa karibu sana na ndugu zake kwa kuwapenda na kuwaunga,wao na watoto wao,haswa ndugu zake wa kike.

Alimuhishimu sana ndugu yake mkubwa Sayyid Ali Badawy na alikuwa na mizani na miko ya mazungumzo mbele yake

WALIMU WAKE

Sharifu Dini alibahatika kukulia katika milango ya Ilimu,Dini na Ucha Mungu na tabia njema,na alikuwa ni katika wanafunzi wa kwanza wa babake mzazi Mwenye Badawy pamoja na ndugu yake Sayyid Ali.

Hali kadhalika alipokea elimu mbali mbali za sharia ya dini kutoka kwa wanazuoni wakubwa waliotajika kama vile:

•Sayyid Abubakar ibn Abdulrahman Al-Hussainy (Mwenye Manswabu),

•Sheikh Muhammad ibn Ali Al Maawy,

•Sheikh Abdallah Abubakar Bakathir (mjombake)

•Sayyid Muhammad ibn Abdallah Al-Rudainy

•Shaikh Al-Amin Mazrui miongoni mwa wengine.

Mwalimu wake mkuu katika taaluma ya Tiba za Kiarabu, elimu ambayo alikuwa ameidhibiti vilivyo,baada ya babake ni ammi yake Sayyid Aidarus ibn Habib Swaleh ambaye alikuwa akimpenda sana. Shariff Dini na Muhammad Bahasan ndio waliokuwa mkono wa kulia wa Al Habib Aidarus katika Usimamizi na Upekeshaji wa Taasisi ya Riyadha.

Katika wasifu wake wa Sharifu Dini, Shaikh Faraj Bwanamkuu, ameeleza kuwa kati ya watoto wa Mwenye Badawy, Sharifu Dini ametanguliwa na Sayyid Ali peke yake kwa kubobea na kufahamu taaluma nyingi za masomo ya dini.

Baadhi ya wanafunzi wenzake aliosoma nao ni; Shaikh Abdallah Bakthir (Kadara), Shaikh Abdallah Khamis (Kidala),

Shaikh Faraj Bwanamkuu, Sharif Said Al-Beidh, Sheikh Bereky,Sayyid Muhammad Saggaf na ndugu yake Sayyid Umar Saggaf pamoja na wengine wengi.

MAISHA YAKE

Kama walivyokuwa Wazee wake, Sharifu Dini alipondokea kwenye shughuli za Elimu na kutangaza Dini. Fauka ya hayo, Mola alimjaaliya vipawa vingi ambavyo vilimvuwa na kumdhihirisha kuwa na ufahamu mpana wa mambo.

Kutokana na mazoea yake ya kupenda kusoma vitabu na ma jarida mbalimbali alimiliki Ufasaha wa lugha za Kiarabu na Kiswahili kwa uzungumzaji na uandishi wa makala na ushairi. Alipenda sana kusoma Tarikhi na Fikra za watu Mash'huri Ulimwenguni hata wasiokuwa waislamu.Mfano Moh'd Ali Jinah,Moh'd Iqbal,Moh'd Abdo, Mahatma Gandhi,Winston Churchill,George Bernard Shaw,Nehru na Wana Falsafa wa Kale kina Ibn Sina,Ibn Rushd na Al Imam Ghazaly. Alithamini tungo na watunzi wa huku kwetu kama Utenzi wa Mwana Kupona na Al Inkishaf

Sharifu Dini alikuwa Tabibu wa kupigiwa mfano. Hakuna shaka kwamba ni wachache wa mithili yake kwenye fani ya tiba,hadi akazawadiwa lakabu aliyostahiki ya 'Daktari' na wale walotambua na kunufaika na Utabibu wake.

Katika lilomfaulisha ni kuwa na usuhuba wa ushauri na kutaka kujua mbinu za Utabibu wa kisasa(wa ki 'hospitali') kwa kutukuwa taaluma kwa madaktari wa hospitali ya Lamu.

Alijifundisha na kuwahi kutumia ala za kupimia joto la mwilini(thermometer)na 'presha'(blood pressure) na alimili pia katika kutibu kwa kuusia miko(kambe)ya vyakula.

Pamoja na kuwa alikuwa na hamu atoe wanafunzi katika fani hini,masharti aloeka ya kuwa mwanafunzi lazima ajifundishe na azowee kutambua magonjwa(diagnosis) na pia lazima ajue 'kutanganya,kuponda na kupika' madawa; yaliwashinda wanafunzi wengi.

Yafaa ijulikane kuwa kazi ya utabibu hakuifanya kwa sababu ya pato, bali mara nyingi akitibu watu bure na kuwaandikia dawa wakanunue wenyewe,ila dawa zilizohitaji vipimo vya hadhari na makini zaidi ndipo alipokuwa akizitengeza mwenyewe.

Alihamasika na kuhamasisha juu ya kadhia za watu wa Palastin na aliongoza Mihadhara na Michango ya kusaidia Wakimbizi wa nchi hiyo.

Sharifu Dini alikuwa mwandishi na mtunzi mahiri. Ameandika makala mengi kuhusu elimu za:

•Falsafa na Tiba, kama alivyokuwa akipenda sana fani za Saikolojia na Sosiolojia. Katika uzungumzi wake hadharani alitofautiana na Makhatibu wengine kwa kuwa Khutba zake zilikuwa na Uzito wa Elimu ya Jamii na Falsafa na kulenga kuukuza Muj'tamai wa kiislamu na alikuwa akisisitiza sana elimu ya tangamano na Tabia njema.Alitangamana na viongozi wa tabaka zote kama walimu wa mashule, watawala, wafanyibiashara na alivaana na watu wa kawaida kwa dhihaka na bashasha

•Vile vile, alikuwa mdadisi wa mambo mbali mbali ya jamii kama siasa, uchumi, elimu, tangamano, mijadala ya dini,fikra ya Biashara ya Ushirika na kadhalika. Si ajabu, katika tungo zake zilizopata umaarufu sana ni tenzi za kitabu chake alichokipa jina la ***Dini na Siasa*** na vitabu viwili vya falsafa vilivyo tafsiriwa kwa lugha ya Kiingereza.

•Hali kadhalika, aliandika ***Kamusi ya Dawa za Miti na Matumizi Yake*** na kitabu kingine alchokiita ***Dawa yako iko Katika Chakula Chako***.

•Ama, kitabu chake kilichotarajiwa kutia fora kwa jina ***Asrarul Hayati***,(Siri za Maisha) kilipotea kwenye shirika la uchapishaji. Baadhi ya makala yake alikuwa akiyapiga chapa mwenyewe kwa mashini ya 'typewriter' na kuwagawia watu bure.

Muda wake mwingi alijishughulisha kuitumikia taasisi ya Riyadha na kutibu halaiki ya watu waliokwenda kutafuta dawa za magonjwa mbali mbali. Makamu yake kama kiungo na nguzo ya usimamizi wa Chuo cha Riyadha yalimfanya asipate nafasi ya kupumua na hamu yake kubwa ilikuwa ni kujaribu kubuni mbinu za kuendeleza Elimu.

Juhudi zake hizo zilimpelekea kufualu kuasisi vyuo na madrasa kadha wa kadha katika miji na vijiji mbali mbali zikiwemo:

• Madrasatul Badawy Kizingitini.

• Madrasatul Jamal Ndau,

• Madrasatul Islahi Matondoni

Na pia ndiye aliyebuni fikra ya kuanzisha mfumo wa ki Madrasa katitka mji wa Malindi.Aliianzisha madrasa hiyo katika nyumba alimokuwa akiishi na akifanya Tiba hapo Malindi kisha ikaguria kwa Sheikh Omar bin Dahman ndipo Swahib yake Abdallah Bakhshuwen akatoa kiwanja watu wa Malindi wakajenga Madrasatul Tahdheeb.Kadhalika,ndiye aliyelibuni Darasa linaloendelea mpaka leo, kila Jumatano alasiri katika Mskiti Mkuu wa Ijumaa akisaidiwa na mnuna wake Sayyid Ahmad Mwenyebaba na Ustadh Salim Basalama

Kenya ilipopata Uhuru, wizara za Utawala na Elimu katika wilaya ya Lamu zilitaka Ushirikiano na Usaidizi wa Riyadha kuanzishwa Shule za 'secular' sehemu mbalimbali za Lamu.Na Shariff Dini kwa rukhsa ya Ami yake Habib Aidarus alishirikiana na Maafisa wa Elimu na Utawala kuwahubiria Waislamu na kuwashawishi wakubali kuanzishiwa maskuli na serikali.Khatua yake hiyo ilimtia kwenye mzozo na baadhi ya viongozi wa madrasa za sehemu fulani,lakini hakurudi nyuma(na hili lilishuhudizwa na Sheikh Muhammad Swalihu Imamu wa Jamia Mosque Nairobi siku ya kufunguliwa jengo lipya la Madrasatul Jamal Ndau miaka michache ilopita)

Yamkini, Sharifu Dini, ndiye mtu wa kwanza Afrika ya Mashariki kubuni mfumo wa kutuma walimu-wanafunzi kutoka chuo cha Riyadha na kuwapeleka sehemu mbali mbali kusomesha kwa mwaka mmoja kama sehemu ya mafunzo yao ya uwalimu, Alitanguliwa na babake tu ambaye alipeleka Walimu waliokamilika sehemu za Tana River na Digo.Mbinu hiyo ndiyo inayotumika sasa katika vyuo vya mafunzo ya uwalimu vya serikali japo huwa ni kwa muda wa miezi michache. (Teaching Practice).

RIYADHA

Sharifu Dini, alibeba majukumu ya kuwasimamia wanafunzi wakigeni katika maslahi yao yote khaswa upande wa ibada, masomo, chakula, malazi na mengineyo akisaidiana na Sayyid Muhammad Bahasan bali kila mara alisafiri katika vijiji vya Tana River, visiwa vya Lamu na vijiji vyote vya mwambao wa Somalia hadi Kismayu ili kuhakikisha mambo ya elimu yamepewa kipao mbele na pia akileta wanafunzi Riyadha kutoka sehemu hizo.

Miongoni mwa sifa za Sharifu Dini kubwa zaidi ilikuwa ni:

•**Kupenda kutunga wakati;** alitukia sana watu kupoteza wakati ovyo khaswa walimu na wanafunzi. Aliamuwa kuwasomesha baadhi ya wanafunzi na ndugu zake kitabu cha ***Minhaju Twalibeen*** wakati wa kabla ya Alfajiri ili wasipoteza muda kwa kulala sana. Aghalabu, alitukuwa nafasi ya ndugu yake Sayyid Ali kuendesha Darasa ya Tafsiri ya Qur'an ya mwezi wa Ramadhan kila kunapotekea haja ya ndugu yake kutokuweko akisaidiana na Sayyid Muhammad Bahasan

•Alisisitiza kudumisha nyendo za Jadi katika kusimamia taasisi za masomo na shughuli za kidini na hakupenda kuwekwa mabadiliko bila ya dharura

•Kwa Upande wa Maulidi ya Riyadha ya Mfungo Sita,alijitahidi kuzipa sherehe za Maulidi sura za Kongamano la kujadili harakati za maendeleo ya Dini,kwa kuhusisha viongozi waliokuwa wakihudhuria kutoka sehemu mbalimbali za East Africa. Kongamano hilo aliliita Muutamar(Conference)ya East Africa

•Pia, alibuni ushirikiano baina ya Riyadha na wanafunzi wa Mashule kwa kuamini kwake kuwa watoto wendao Maskuli lazima wakurubishwe,wasitengwe.Mfano ni wale wanafunzi wa Lamu Primary kwenye miaka ya 1950-1960.Hawa aliwaekea darasa ya Fiqhi na Tabia Njema Msikiti wa Ras Kop.Vile vile wanafunzi wa shule ya Upili ya Bweni ya Lamu Boys wakati wa uongozi wa Maalim Abdallah El-Lamy na Maalim Hussain Soud El-Maawy. Wanafunzi wa shule hiyo walipangiwa kwenda Riyadha kusoma masomo ya Dini baina ya nyakati za magharibi na ishaa.

Aliusia sana, walimu wawe ni kielelezo chema kwa wanafunzi katika swala za jamaa, nyuradi za alfajiri na jioni na kwenye shughuli zote za twariqa na akisisitiza ***kuwa elimu ya mtu huonekana kwenye tabia na matendo yake***.

WATOTO WAKE:

WA KIUME

1.Shariff Ali Dini (Mwenye Ali) (marehemu) (Alisomesha Lamu,Ndau,Kismayu,Jinja na Tanzania Bara)

2.Ustadh Alwy Dini(Alisomesha Matondoni,Riyadha,Kilifi na Tanzania Bara)

3.Abubakar Dini (alikuwa Mwalimu na Mwanasiasa Mbunge)

4.Ahmad Badawy (Alitokana na kizazi cha Shariff Nur Al Nadhir wa Ndau)(alifariki mdogo)

WA KIKE

1.Sayyidah Zahra Dini (marehemu) (Mamao kina Sheikh Bahasan)

2.Sayyidah Fatma Dini (marehemu) (Mamao kina Ghalib Muhdhar Al Hussein)

3.Sayyidah Maimuna Dini (Mamao kina marhum Moh'd Swafi)

4.Sayyidah Twaiba Dini (mkewe Abdulrahman Badawy)

5.Sayyidah Amina Dini (mkewe Hajj Abdulrazak)

6.Sayyidah Umu Hani Dini (mkewe Shihabdin Khitamy)

Mola alimuwafikia kutumia umri wake mrefu na wakati wake wote kwa kuipotolea kwenye kazi ngumu ya kutangaza Elimu na Dini tukufu ya uislamu mpaka alipopata mtihani wa maradhi uliomlazimisha kubaki kitandani kwa muda wa miaka minne.

Kwa wakati mchache kwenye maisha yake,kwenye Ubarobaro wake aliwahi kujitosa wakati wa shida ya vyakula na vikwazo ya vibali za Usafirishaji kwa kufanya biashara ya kununua chakula kwa magendo na kusafirisha kwa jahazi baina ya Mombasa,Malindi na Lamu. Lengo ilikuwa ni kusaidia Umma dhidha ya shida na janga la njaa.

Baada ya kuuguwa na huku akisubiri na kushukuru kadari ya Mola, Sharifu Dini, aliaga dunia mwaka wa 1986 AD (1406 AH) katika mji wa Malindi akiwa kwenye mikono ya watoto, ndugu na jamaa zake. Amezikwa kwenye makaburi ya mashemeji zake Washela karibu na Msikiti wa Abdallah Hussein, Shella, Malindi.

Mola aiweke roho yake mahali pema pamoja na wazee wake na wema wengine peponi na atuafiqie kufuata nyayo zake katika kuitumikia Riyadha na Dini kwa Jumla.. Ameen

Imetayarishwa na :

IDARA KUU YA RIYADHA MOSQUE & ISLAMIC CENTRE, LAMU.

Baadhi ya Maalumati yalipatikana kwa Sayyid Abdulrahman Khitamy, Sayyid Ahmad Mwenyebaba,Sheikh Faraj Bwanamkuu,Sheikh Abdallah Kadara,Bwana Kifeli,Maalim Salim Khamis Baakabe,Ustadh Harith,Sheikh AbdulAziz Mahmud Albakary,Maalim Amir Awadh,Maalim Hussein Soud Al Maawy,Sheikh Rashid Ali Riyamy